

# MWENGE WA UHURU DODOMA MJINI 2018

Mwenge wa Uhuru leo umeingia katika Wilaya ya Dodoma Mjini. Majira ya asubuhi mwenge huo ulikabidhiwa kwa Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini Mh. Patrobas Katambi kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Chemba Mh. Simon Ezekiel Odunga katika eneo la Makutupora. Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2018 unakimbizwa na vijana sita wakakamavu wakiongozwa na Mhandisi Charles Francis Kabeho.

Baada ya kukabidhiwa kwa Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Mwenge wa Uhuru umekimbizwa umbali wa kilometa 81, ambapo umepitia miradi saba na umefanya shughuli za kuweka mawe ya msingi, kuzindua na kutembelea miradi hiyo. Miradi yote iliyopitiwa na Mwenge wa Uhuru, imekaguliwa kwa umakini na kukubaliwa kuwa imekidhi viwango (standards) na thamani ya pesa (Value for Money).

Aidha miradi iliyopitiwa na Mwenge wa Uhuru ni Mradi wa Matofari na ujenzi Kikosi cha Jeshi la Kujenga Taifa JKT Makutupora, Mradi wa Barabara (TARURA), Mradi wa Kituo cha Mafuta GP 88 (Makulu), Mradi wa Karakana ya Ufundi Seremala (VETA Dodoma), Mradi wa Ujenzi wa Maabara (Sekondari ya Dodoma) na Upanuzi wa Majengo ya Huduma za Afya na ujenzi wa nyumba ya mtumishi katika Kituo cha Afya Makole. Miradi yote imegharimu jumla ya kiasi kisichopungua shilingi bilioni 5.2.